**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI**

*Email:* marcochupa@yahoo.com
Phone No. 0763241626

SHULE YA SEKONDARI MWAMALOLE,
S.L.P 203,
**MEATU.**

KUMB. NA. MSS/S.2341/JI/VOL.16/2020/01 15, DECEMBER, 2020.

JINA LA MWANAFUNZI--------------------------------------------------

S.L.P.44,

**MEATU.**

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWAMALOLE, WILAYA YA MEATU, MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021.

## 1.0 UTANGULIZI;

Ninafurahi kukuarifu ya kuwa umechaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021,** shule ya sekondari **Mwamalole** ipo umbali wa km **52** kusini mwa mji wa Mwanhuzi.

Mhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**, unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021**, na mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/01/2021**, ndani ya siku tano tu.

## 2.0 MAMBO YA KUZINGATIA;

### 2.1 SARE ZA SHULE;

a) **WAVULANA**; Suruali rangi ya damu ya mzee yenye malinda mawili, shati nyeupe mikono mifupi, soksi nyeusi, tai ndefu rangi yake ni kama suruali na viatu vya ngozi, vyeusi vya kufunika miguu visivyo mchongoko wala vyenye sole nene.

b) **WASICHANA**; Sketi rangi ya damu ya mzee yenye kuvuka magoti na inayokutana na soksi iliyo na malinda manane, shati nyeupe mikono mifupi, tai ndefu rangi yake ni kama sketi, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufunika miguu visiwe na kisigino kirefu.
**NB:-** kwa msichana mwenye hijabu ifanane rangi na sare za shule, naambatanisha na sampuli ya kitambaa na rangi husika.

c) Sare ya michezo kwa shule hii ni Bukuta rangi ya blue kwa wavulana na Tshirt ya blue kwa wasichana ni suruali ya Traka na Tshirt vyote rangi ya blue.

2.2 Vifaa muhimu vya darasani ni:

- Daftari kubwa 10 (**counter books-Quire 2**)
- Kalamu 2 za wino na pencil 2
- Mkebe wa hesabu (**Mathematical set 1**)
- Begi la daftari na siyo Rambo.

2.3 Kwa mzazi ambaye mwanae anatoka mbali ahakikishe anampatia usafiri wa uhakika ili asichelewe au kukosa kufika shuleni.

**3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa **sheria Na. 10 ya mwaka 1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni;

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kushiriki kwa makini darasani na kujisomea baada ya muda wa darasani kuisha.
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira mengine ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote
h) Kutunza mali za umma na
i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

**3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

a) Wizi b) Uasherati na Ushoga. c) Ubakaji. d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika. e) Kupigana au kupiga.

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g) Kudharau bendera ya Taifa.

h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.

i) Kuoa au kuolewa.

j) Kutoa mimba

k) Kugoma, Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

m) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwana kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi ;

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0 Tafadhari soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

……………………………………………

**Marco Ng'wendamunkono**

**MKUU WA SHULE.**

HEADMASTER
MWAMALOLE SECONDARY SCHOOL
MEATU

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE.**
**SEHEMU 1. (IJAZWE NA MWANAFUNZI)**

MKUU WA SHULE ________________
SHULE YA SEKONDARI MWAMALOLE
S.L.P. 232,
MEATU -MWANHUZI

Ndugu;

YAH: **KUKUBALI MAAGIZO NA SHERIA ZA SHULE**

Mimi ……………………………niliyechaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza katika shule yako mwaka huu wa …………..kutoka shule ya Msingi ……………….Wilaya ………………..Mkoa ……………………Nilizaliwa tarehe ………Mwezi ……………..Mwaka kutokana na barua niliyopokea yenye kumb. Na ………………………..nimeisoma na kuyaelewa maagizo na sheria za shule. Hivyo nimekubali/sijakubali kuchukua nafasi hiyo ya kujinga na kidato cha ……………mwaka …………..Na nitayatekeleza/sitayatekeleza (kata isiyostahili) maagizo hayo na maelekezo mengine nitakayopewa shuleni.

Naahidi kujifunza masomo yote kwa bidii na kufanya mitihani na pia nitakuwa mtiifu, mwaminifu, mvumilivu na mkweli. Uzembe, uvivu, utoro, udanganyifu, kushawishi au kujiunga katika Migomo kwangu ni mwiko.

Atakayehusika na taarifa zangu jina la Mzazi/Mlezi ……………………………Anuani Yake ni ………………………………kazi yake ni ………………….. ……………………anapokaa …………………………

**Sahihi ya Mwanafunzi ………………………………………..**

**Jina kamili la Mwanafunzi …………………………………….**

**Tarehe……………………**

**SEHEMU 2: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)**

Ndugu;

YAH: **UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI**

Kabla ya kujaza fomu hii hakikisha unaisoma na kuielewa vizuri barua yetu yenye

Kumb. Na. ……………………………………………………………………………………

Mimi ……………………………ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi

…………………………………

aliyechaguliwa kujiunga na shule yako kupitia barua yako yenye

Kumb. Na. ……………………………ya tarehe ………………………ikiwa ni pamoja na maelekezo ya mahitaji ya shule, sheria za shule, mwanafunzi kurudi shuleni zamu kwa kipindi cha likizo, kuhudumia miradi ya shule. Nayakubali/siyakubali maelezo haya na nitayatekeleza/sitayatekeleza kwa wakati unaotakiwa (kata isiyohusika).

Pia ninaahidi kutuma taarifa za matukio yote ya dharau kwa mtoto kupitia ofisi ya Mkuu wa Shule (kama magonjwa, vifo N.K).

Nitakuwa/sitakuwa tayari kufika shuleni endapo nitaitwa na uongozi wa shule kufuatia utovu wa Nidhamu utakaokuwa umefanywa na mtoto wangu.

Taarifa zote zinazohusu mtoto wangu nitumiwe kwa anuani ifuatayo

…………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

Jina la Mzazi ……………………………………………………

Sahihi ya mzazi/mlezi ……………………………………………..

Simu namba ……………………………………………………..

Tarehe………………………………………………………………

**NB**: Karatasi/fomu hii itatolewa na kuhifadhiwa kwenye jarada la mwanafunzi mara tu atakaporipoti na kusajiliwa rasmi.

**MWAMALOLE SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL REPORT FORM FOR STUDENT**

**PART I STUDENTS PERSONAL DETAILS**

Student Names: …………………………………………
Age: ……………………………….
Sex: ……………………………….
PART II MEDICAL REPORT
Area you suffering or have suffered from any of the following? Indicate Yes or No

1. Tuberculosis ……………………………………………………………………………
2. Asthma …………………………………………………………………………………
3. Rheumatic fever …………………………………………………………………………
4. Allergic disorders ………………………………………………………………………..
5. Heart disease ……………………………………………………………………………..
6. Dysentery …………………………………………………………………………………
7. Viscose veins ……………………………………………………………………………..
8. Kidney diseases …………………………………………………………………………..
9. Diabetes ……………………………………………………………………………………
10. Epilepsy ……………………………………………………………………………………
11. Deformity …………………………………………………………………………………
12. Mental illness ……………………………………………………………………………..
13. Eye Disorder ………………………………………………………………………………
14. Ear, Nose or Throat disorder ……………………………………………………………...
15. Skin diseases ………………………………………………………………………………
16. Anemia ……………………………………………………………………………………
17. Gynecological disorder ……………………………………………………………………

**PART III: CONCLUSION**

I have personally examined Mr. /Miss ……………………………………and consider that he/she is
Physically and mentally fit/not fit to be admitted to the school for studies.
NAME: ………………………………………………………………………

TITLE ……………………………………….

QUALIFICATIONS ………………………..

SIGNATURE ……………………………..

OFFICIAL STAMP ………………………..

DATE …………………